

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Simu ya mdomo: 255 22 2460 735/2460 706-8  
FAKSI: 255 22 2460 735/700  
Simu pepe: met@meteo.go.tz  
Tovuti: www.meteo.go.tz

S.L.P. 3056  
DAR ES SALAAM

Unapojibu tafadhali nakili:  
**Ref. No.: TMA/1622**

3 Machi, 2016

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI  
MWELEKEO WA MVUA KWA KIPINDI CHA MACHI - MEI 2016 NCHINI**

**A: UTANGULIZI**

Taarifa hii inatoa tathmini ya mvua za vuli (Oktoba - Disemba) 2016 na mwelekeo wa mifumo ya hali ya hewa na mvua kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Mei, 2016(Masika).



**Dondoo muhimu Mvua za Masika Machi-Mei, 2016**

**1. Mwelekeo wa mvua za Masika kwa kipindi cha Machi-Mei, 2016 unaonesha kuwa;**

Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi 2016 katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Viktoria na kusambaa katika maeneo mengine yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Mvua hizo zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo machache yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Mvua za msimu zinazoendelea zinatarajiwa kunyesha katika kiwango cha wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi.

**2. Athari zinazotarajiwa**

Upatikanaji wa malisho unatarajiwa kuwa wa kuridhisha hususan katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Viktoria na Nyanda za juu kaskazini Mashariki. Hali ya unyevunyevu wa udongo inatarajiwa kuwa ya kutosheleza shughuli za kilimo katika maeneo mengi. Hata hivyo, mvua za juu ya wastani zinazotarajiwa kunyesha zinaweza kusababisha hali ya unyevunyevu wa udongo kupita kiasi hivyo kuathiri mazao. Mlipuko wa magonjwa kama vile Malaria unatarajiwa kujitokeza baada ya kunyesha kwa mvua hizo. Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha mafuriko.

## **B: TATHMINI YA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA – DISEMBA, 2015**

Katika msimu wa mvua za Vuli za mwezi Oktoba hadi Disemba 2015, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za wastani hadi juu ya wastani isipokuwa maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini mashariki na Pwani ya Kaskazini hususan mkoa wa Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, ambayo yalipata mvua za chini ya wastani na mtawanyiko wake haukuwa wakuridhisha katika kipindi hicho. Hata hivyo, kutokana na uwepo wa El Niño hali ya mvua iliendelea katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka katika kipindi cha miezi ya Januari na Februari 2016.

El Niño iliyojitokeza mwaka 2015 na kuendelea hadi mwaka huu 2016 ilisababisha ongezeko kubwa la joto hapa nchini. Viwango vya joto vilivyojitokeza vilifikia hadi nyuzi joto 36 hususan katika maeneo ya ukanda wa Pwani na yale ya Nyanda za juu Kaskazini Mashariki, kiwango ambacho ni cha juu ya wastani kwa takribani nyuzi joto 1.7 hadi 2.0. Tofauti hiyo ya hali ya joto ni kubwa ikilinganishwa na viwango vilivyowahi kupimwa katika miaka mingi iliyopita katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Hali ya Hewa duniani (WMO) ongezeko la joto pia limejitokeza katika maeneo mengine duniani.

**Kanda ya Ziwa Victoria:** Maeneo mengi ya mikoa ya Mwanza, Geita na Mara yalipata mvua za juu ya wastani ambapo mikoa wa Shinyanga na Kagera ilipata mvua za wastani.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki:** Maeneo ya mikoa ya Arusha na Manyara yalipata mvua za juu ya wastani. Wakati mikoa ya Kilimanjaro na maeneo ya kusini mashariki mwa mkoa wa Manyara yalipata mvua za wastani hadi chini ya wastani.

**Pwani ya kaskazini pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba:** Vituo vya Tanga, Handeni na Mlingano vilipima mvua za juu ya wastani, ambapo maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua za Wastani. Maeneo ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam yalipata mvua za chini ya wastani.

**Nyanda za juu kusini magharibi:** Mvua za wastani hadi juu ya wastani zilipimwa katika maeneo ya Sumbawanga, Iringa, Njombe Songwe na kusini mwa mkoa wa Mbeya. Hata hivyo maeneo machache yalipata mvua za chini ya wastani.

**Kanda ya magharibi:** Maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora yalipata mvua za wastani hadi juu ya wastani.

**Pwani ya kusini:** Maeneo ya mikoa ya Mtwara na Lindi yalipata mvua za chini ya wastani.

**Kanda ya kati:** Mikoa ya Singida na Dodoma ilipata mvua za wastani hadi juu ya wastani, isipokuwa maeneo machache ya mkoa wa Dodoma (Hombolo) yalipata mvua za chini ya wastani.

**Kanda ya kusini:** Mvua za wastani hadi juu ya wastani zilipimwa katika kituo cha Songea.

## **C: MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya joto imeendelea kuwepo katika eneo la bahari ya Hindi, kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki na Tropikali ya kati ya Bahari ya Pasifiki kwa kipindi cha mwezi Februari, 2016. Hali ya joto inatarajiwa kuendelea katika eneo la Tropikali ya kati ya Bahari ya Pasifiki, ikiashiria kuendelea kuwepo kwa El Niño katika kipindi cha msimu wa *Masika* 2016. Hali ya joto eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi inatarajiwa kuendelea, ambapo eneo la mashariki linatarajiwa kuwa na joto zaidi katika msimu wa *Masika*, 2016. Hali ya joto kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) inatarajiwa kuendelea katika kipindi cha mwezi Machi na kupungua katika miezi ya Aprili na Mei, 2016.

Hali hiyo ya kupungua kwa joto katika pwani ya Angola inatarajiwa kuongeza msukumo wa hewa yenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya nchi hadi bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine, hali hii itachangia kupunguza msukumo wa upepo wenye unyevunyevu kutoka bahari ya Hindi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya joto katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi kunatarajiwa kuchangia kuwepo kwa matukio ya vimbunga, hivyo kuathiri hali ya mvua za *Masika* 2016.

## **D: MWELEKEO WA MVUA ZA MACHI - MEI 2016**

Kutokana na mwelekeo wa mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa, mvua za Machi hadi Mei, 2016 zinataraajiwa kuwa kama ifuatavyo:-

### **(i) Mvua za *Masika* (kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua)**

Msimu wa mvua za *Masika* katika kipindi cha miezi ya Machi hadi Mei, 2016 ni mahususi katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara), pwani ya kaskazini, (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro-kaskazini pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga) na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua hizo zinataraajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani kwa maeneo mengi ya ukanda huo isipokuwa maeneo ya kusini mwa ukanda huo yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani.

Mwelekeo wa msimu wa mvua za *Masika*, 2016 ni kama ifuatavyo:-

### **Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):**

Mvua zinataraajiwa kuanza wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2016 katika mikoa ya Kagera na Mara na kusambaa katika mikoa ya Geita, Mwanza, Shinyanga na Simiyu katika wiki ya pili ya mwezi Machi 2016. Mvua zinataraajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara na kaskazini mwa mkoa wa Geita. Kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, kusini mwa Geita na Simiyu, pamoja na mkoa wa Shinyanga mvua zinataraajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani.

### **Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro-kaskazini pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba):**

Mvua zinataraajiwa kuanza wiki ya pili hadi ya tatu ya mwezi Machi, 2016 na zinataraajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo ya kaskazini na mashariki mwa mkoa wa Tanga ; na Visiwa vya Unguja na Pemba. Mvua zinataraajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro pamoja na maeneo ya kusini magharibi mwa mkoa wa

Tanga.

**Nyanda za juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili hadi tatu ya mwezi Machi, 2016. Mvua hizo zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Arusha na Kilimanjaro pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Manyara; na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya mkoa wa Manyara na kusini mwa mkoa wa Arusha.

**(ii) Mvua za Msimu (Novemba – Aprili) kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua.**

Mvua za msimu (Novemba hadi Aprili) ni mahususi kwa maeneo ya Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa), kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma), nyanda za juu kusini-Magharibi (Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na kusini mwa Morogoro), kusini mwa nchi na pwani ya kusini (mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara). Mvua hizo zilianza mwezi Novemba 2015 na zinatarajiwa kuendelea hadi mwezi Aprili, 2016. Katika maeneo hayo mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi.

**Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa):**

Katika kipindi kilichobaki cha msimu, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa kuisha mnamo wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2016.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):**


Katika kipindi kilichobaki cha msimu, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa kuisha mnamo wiki ya kwanza ya mwezi Aprili, 2016.

**Nyanda za juu Kusini Magharibi: (Mikoa ya Mbeya, Songwe Iringa, Njombe na kusini mwa Morogoro):**

Katika kipindi kilichobaki cha msimu, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa kuisha mnamo wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2016 katika maeneo ya mikoa ya Mbeya, Songwe na Njombe na zinatarajiwa kuisha katika wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2016 katika maeneo ya mkoa wa Iringa.

**Maeneo ya kusini na pwani ya kusini (Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara)**

Katika kipindi kilichobaki cha msimu, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa kuisha mnamo wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2016.



***Izingatiwe kuwa pamoja na kuwepo kwa uwezekano wa matukio ya mvua kubwa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua juu ya wastani, hali hiyo pia inaweza kujitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani.***

*Matukio ya Vimbunga katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi yanatarajiwa kuathiri mwenendo wa mvua za msimu wa Machi hadi Mei, 2016 hapa nchini.*

**E: ATHARI NA USHAURI**

Katika Msimu wa mvua za Masika hali ya mvua katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Viktoria, Nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na maeneo ya machache ya Mikoa ya Tanga na Kisiwa cha Pemba inatarajiwa kuwa ya wastani hadi juu ya wastani. Maeneo mengi ya nchi hususan Nyanda za juu kusini Magharibi Magharibi mwa nchi, Kanda ya kati na pwani ya kusini yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Athari ya mvua hizo pamoja na ushauri kwa baadhi ya sekta za kiuchumi na kijamii yameainishwa na TMA ikishirikiana na wadau kama ifuatavyo:-

**Kilimo na Usalama wa Chakula**

Hali ya unyevunyevu wa udongo inatarajiwa kuwa ya kutosheleza shughuli za kilimo katika maeneo mengi. Hata hivyo, mvua za juu ya wastani zinazotarajiwa kunyesha zinaweza kusababisha hali ya unyevunyevu wa udongo kupita kiasi hivyo kuathiri mazao. Wakulima wanashauriwa kuendelea na shughuli za kawaida za kilimo katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu za kuongeza uzalishaji, kupanda mazao na miti pamoja na kuzingatia ushauri wa wataalam wa kilimo katika matumizi sahihi ya ardhi na mbegu. Hata hivyo, Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chini ya wastani upungufu wa unyevunyevu wa udongo unaweza kujitokea hususan katika vipindi vya kukosekana kwa mvua. Mbinu za kuhifadhi, maji pamoja na kuthibiti ubora wa mavuno zinapaswa kuzingatiwa. Wakulima waendeleo kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika

kutekeleza shughuli zao.

### **Malisho, Maji kwa ajili ya mifugo na Wanyama pori**

Malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na wanyama pori yanatarajiwa kuwa ya kutosheleza katika maeneo mengi ya ukanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na mkoa wa Tanga na kisiwa cha Pemba ambapo mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa. Hata hivyo, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani upungufu wa malisho na uzalishaji wa mifugo na samaki unaweza kujitokeza. Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kufuata ushauri wa wataalam sambamba na kuzingatia taarifa za ziada (update) za utabiri zinazotolewa.

### **Maliasili na Utalii**

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani Mamlaka za usimamizi wa shughuli za utalii na hifadhi za wanyamapori zinashauriwa kuchukua hatua stahiki katika kuzuia uharibifu wa miundombinu ndani ya hifadhi dhidi ya adhari za mvua zinazotarajiwa. Katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa ziwa Viktoria wachimbaji wadogo wa madini wanahimizwa kuchuka tahadhari stahiki katika kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na maji pamoja na mafuriko kuingia ndani ya migodi.

### **Maji na Nishati**

Katika maeneo yanayotarajiwa kapata mvua za wastani hadi chini ya wastani taratibu za kuvuna na kuhifadhi maji zizingatiwe hususan kwa matumizi ya uzalishaji wa nishati ya umeme wa maji. Aidha, njia mbadala za uzalishaji nishati zizingatiwe ili kufanikisha upatikanaji endelevu wa nishati ya umeme.

### **Mamlaka za Miji**

Kutokana na vipindi vya mvua kubwa vinavyotarajiwa kujitokeza Mamlaka za miji na Jiji zinashauriwa kuchukua hatua kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanyakazi katika kiwango cha kutosha ili kuepusha maji kutuama na kusababisha mafuriko na uharibifu wa miundombinu, upotevu wa maisha na mali hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chini ya wastani kwa sababu vipindi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kufanya uhakiki wa Miundombinu pamoja na kujiandaa kupunguza adhari zinazoweza kujitokeza katika maeneo mbalimbali.

### **Sekta ya Afya**

Mvua za *Masika* zinazotarajiwa zinaweza kusababisha milipuko ya magonjwa hivyo ushauri unatolewa kwa jamii na sekta husika kuchukua hatua stahiki kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

### **Menejimenti ya Maafa**

Mamlaka za maafa na wadau wengine wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utunzaji wa mazingira, kuandaa mipango ya kupunguza na kukabiliana na maafa.

### **Vyombo vya habari**

Katika kukabiliana na taarifa zisizo rasmi au zisizothibitishwa zinazoweza kujitokeza vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa

kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Aidha, vyombo vya habari vinashauriwa kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii. Jamii kwa ujumla nayo inashauriwa kufuatilia na kuzingatia taarifa sahihi za hali ya hewa na mirejeo yake kupitia vyombo vya habari.

Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

*Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu(miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.*

***Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania Itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini.***

Imesainiwa na:

Dkt Agnes L. Kijazi

**Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**